OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI
SHULE YA SEKONDARI SADANI

S.L.P 284,
MAFINGA.

10 December 2020

KUMB NA SASS/ F.I ADM/ VOL II/……..

Ndugu

……
……

Salamu,

YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE KIDATO CHA I, 2021</u>

Wanajumuiya wa shule ya sekondari Sadani wanakupongeza sana kwa kuchaguliwa kwako kuendelea na masomo ya sekondari katika shule yetu. Ni muhimu uelewe kuwa serikali yetu imekupa nafasi hii ili kukuandaa uweze kulitumikia Taifa letu hapo baadaye. Hivyo itakupasa kuitumia nafasi hii **ADIMU** kwa bidii na kwa moyo wako wote ili usiisaliti imani iliyowekwa kwako na Taifa. Shule hii ni ya kutwa na inawapokea wasichana na wavulana.Kauli mbiu yetu ni;

"**QUALITY EDUCATION IS OUR PRIORITY**"

KUFUNGUA SHULE

Shule itafungua tarehe 11 **Januari 2021** na wewe unatakiwa uje kuripoti kuanzia **tarehe 8 Januari 2021** saa mbili asubuhi ili uandikishwe tayari kuanza masomo tarehe 11 **Januari 2021**. Siku ya kuja kuandikishwa kila mwanafunzi aje na mzazi au mlezi wake kwa ajili ya maelekezo zaidi.

A. WASICHANA

1. Madaftari makubwa (counterbooks) 10
2. Madaftari madogo 10.
3. Mkebe (mathematical set) 1
4. Vifaa vya kuandikia (peni, penseli na mfuto, rula)
5. Dictionary.
6. Sketi mbili, moja rangi nyeusi na nyingine rangi ya kijani jeshi. Sketi hizo

Zishonwe vizuri zikiwa na urefu unaopita magoti na malinda kumi na mbili.

7. Blauzi mbili nyeupe zisizo na urembo wowote.
8. Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na urembo wowote na vyenye visigino vifupi.
9. Soksi nyeupe jozi mbili.
10. Sweta la kijani kibichi lenye shingo ya ‘ V’.
11. Nywele Kama sare ya shule zinatakiwa ziwe fupi na safi wakati wote.
12. Si ruhusa kuvaa mapambo kama vile hereni,bangili,viatu vya ghorofa,pete na vibanio vya nywele,wala kupaka rangi ya kucha wala midomo au nyusi wakati wote wa shule.

B. WAVULANA

1. Madaftari makubwa (counterbooks) 10.
2. Madaftari madogo 10.
3. Mkebe (mathematical set) 1
4. Vifaa vya kuandikia (peni,penseli na mfuto,rula).
5. Dictionary
6. Suruali mbili moja rangi nyeusi na nyingine ya kijani jeshi. Suruali zote zishonwe na ziwe pana chini na zivaliwe kiunoni kwa mkanda.
7. Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na urembo na viwe na visigino vifupi.
8. Soksi nyeusi jozi mbili.
9. Sweta rangi ya kijani kibichi lenye shingo ya` V’.
10. Nywele kama sare ya shule zinatakiwa ziwe fupi na za kuchana. Ni marufuku kunyoa kipara au kufuga ndevu. Kucha ziwe fupi na safi wakati wote na usivae mapambo yoyote shuleni, kofia, na mizura haziruhusiwi.

N.B: Kila mwanafunzi anatakiwa kuja cheti cha kuzaliwa.

C. YAFUATAYO NI MAKOSA AMBAYO BAADA YA KUTHIBITISHWA YANA WEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

1. Wizi
2. Uasherati, ubakaji na ushoga
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
4. Uvutaji wa bangi
5. Makosa ya jinai
6. Kupigana au kupiga.
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
8. Kuoa au kuolewa.
9. Kudharau Bendera ya Taifa.
10. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
11. Kutoa mimba.
12. Kukataa adhabu kwa makusudi.
13. Kugoma,kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu.
14. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi

15. Kulala nje ya shule bila ruhusa

N.B: Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na cheti cha kuzaliwa.

Kabla ya kuanza safari ya kuja shuleni tafadhali soma kwa makini maelezo yote na ukamilishe mahitaji yote ikiwa ni pamoja na kujaza fomu zilizoambatanishwa. Mwisho nakutakia maandalizi mema na safari njema ya kuja hapa sekondari Sadani.

KARIBU SANA

_____

MPAMBWE PAUL

MKUU WA SHULE

KUMBUKUMBU MUHIMU ZA MWANAFUNZI

A. MWANAFUNZI NA WAZAZI/WALEZI WAKE

i. Jina la mwanafunzi.....
ii. Tarehe ya kuzaliwa.....mahali.....
iii. Jina la baba.....yu hai/amefariki.....
iv. Mahali anakoishi;

Kijiji/Mji.....kata.....tarafa.....
v. Kazi ya baba.....
vi. Anwani yake.....simu.....
vii. Jina la mama.....yu hai/amefariki.....
viii. Mahali anakoishi;

Kijiji/Mji.....kata.....tarafa.....
ix. Kazi ya mama.....
x. Anwani yake.....simu.....
xi. Jina la mlezi.....
xii. Mahali anakoishi;

Kijiji/Mji.....kata.....tarafa.....
xiii. Anwani yake.....simu.....

B. NDUGU WA KARIBU WA MWANAFUNZI

NA	JINA	UHUSIANO	NA.YA SIMU/ANWANI
1			
2			
3			
4			
5			
6			

C. AHADI YA KUFUATA SHERIA NA TARATIBU ZASHULE(MWANAFUNZI)

Mimi.....naahidi kufuata sheria,kanuni na taratibu za shule hii na kutekeleza maagizo yote yatakayotolewa na uongozi wa shule wakati wote nitakaokuwa ndani na nje ya shule.Sitajihusisha na migomo,fujo wala makosa ya jinai.
Sahihi.....tarehe.....

D. AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi.....ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi aliyeweka ahadi hapo juu,naahidi kumpatia ada ya shule,michango na mahitaji yote yanayotakiwa kujiunga na shule hii.

Sahihi..... Tarehe .....

PRESIDENT'S OFFICE-REGION ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
MUFINDI DISTRICT COUNCIL

SADANI SECONDARY SCHOOL

MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by medical officers in a recognize Hospital in respect of all new entrants to Sadani Secondary School.

Full name.....
Age.....

1. Blood comment
   (Red&White).....
2. Urine examination.....
3. Stool examination.....
4. Syphilis test.....
5. T.B test.....
6. Ear test.....
7. Eye test.....
8. Speen.....
9. Abdominal.....
10. Additional information or any other physical, hereditary or infectious disease:
    .....
    .....
    .....

    Treatment after examination:

.....
.....

MEDICAL CERTIFICATE

I certify that the abovementioned has been examined and found fit to pursue for further education.
Signature.....
Designation.....
Station.....

(Official stamp).....

Date.....

NB: Fomu hii ijazwe na Mganga katika hospitali inayotambulika na Serikali.

SHULE YA SEKONDARI SADANI.

A. MAHITAJI KWA WANAFUNZI WANAOPENDA KUKAA HOSTEL "IKUMBUKWE KUWA NAFASI YA HOSTELI IPO KWA WASICHANA NA WAVULANA WENYE JUHUDI KATIKA MASOMO NA WENYE MAADILI MEMA."

I. SARE

a. Kwa wasichana wanaokaa hosteli wanatakiwa kuwa na sare maalumu (Shamba dress) ambayo ni gauni la rangi ya zambarau 1 kwa ajili ya kazi za nje, liwe refu lenye marinda. T-shirt moja rangi ya blue yenye kola na nembo ya shule (T-shirt aina ya Form six). T-shirt zote zinapatikana shuleni kwa bei ya Tshs 13000/= (Elfu kumi na tatu tu).

b. Kwa wavulana wanaokaa hosteli wanatakiwa kuwa na sare maalumu (Shamba dress) ambayo ni suruari ya rangi nyeusi au ya kijani jeshi moja pamoja na T-shirt1 rangi ya blue yenye kola na nembo ya shule (T-shirt aina ya Form six). T-shirt zote zinapatikana shuleni kwa bei ya Tshs 13000/= (Elfu kumi na tatu tu). Suruali zote zishonwe vizuri na zivaliwe kiunoni kwa mkanda kwa ajili ya kazi za nje,

II. MAHITAJI YA BWENI

a. Blanketi moja.
b. Shuka mbili za rangi ya pinki au bluu bahari (light blue).
c. Tochi ya betri mbili
d. Ndoo au dishi kwa ajili ya kufulia, kuchotea maji na kuogea
e. Godoro la futi mbili na nusu.
f. Uwe na sanduku linalofunga vizuri kwa kuhifadhi nguo na vitu vyake.
g. Vyombo vya chakula kama sahani,bakuli,kijiko,jagi na kikombe.
h. Madaftari makubwa kumi na moja pamoja na kalamu za wino.
i. Mkebe wa zana za hisabati(mathematical set) mmoja.
j. Nguo za michezo (track suti nyeusi yenye mstari mweupe).
k. Raba kwa aajili ya michezo.
l. Aje na vifaa vya usafi ambavyo ni; Ndoo ndogo moja, Soft bloom moja, Hard bloom moja, na Squeezer moja.

NB: Vifaa vinapatikana maeneo ya shuleni kwa bei nafuu.

III. CHAKULA NA PANGO

Kila mwanafunzi wa hosteli anatakiwa kutoa sh.**500,000/=** (Mia tano elfu tu) kwa ajili ya chakula na pango kwa mwaka. Unaweza kutoa kwa awamu mbili kwa mchanganuo ufuatao:

Januari Tsh. 250,000/=
Julai Tsh. 250,000/=

Lipa malipo ya hostel kwa; **Account Name**; Akaunti ya Wazazi Sadani,
Account No. 0152372326700 **CRDB.**
Pesa taslimu haitapokelewa shuleni.

NB: Mwanafunzi atakayeshindwa kufikisha wastani wa hamsini (50) katika mitihani yake au baada ya kuthibitishwa kuwa ana makosa ya kinidhamu na ukiukwaji wa sheria zashule ataondolewa bwenini.

KWA MWANAFUNZI WA HOSTELI NI SHARTI AFUATE KANUNI ZIFUATAZO:

1. Kusoma kwa bidii, Juhudi na maarifa wakati wote.
2. Kufikisha wastani wa alama 50%.
3. Kuwa msafi binafsi, mavazi, chumba na mazingira anayoishi.
4. Kulinda na kutunza mali za shule.
5. Kutojihusisha na urafiki wa kimapenzi.
6. Kutoa taarifa kwa matron, mwalimu, au mkuu wa shule tabia yoyote mbaya ambayo mwanafunzi mwenzake anaifanya.
7. Kutomiliki simu.
8. Kutotoka nje ya shule bila ruhusa.
9. Kutolala nje ya hosteli bila ruhusa ya mwalimu.
10. Kutowatishia, kutukana, kashfu, dharau wanafunzi wenzake.

NB: Ikiwa mwanafunzi wa hosteli atakiuka moja kati ya kanuni hizo ataondolewa hosteli.

AHADI YA MWANAFUNZI KUTII NA KUFUATA MASHARTI YA HOSTELI

Mimi _____ wa kidato cha _____

Ninaahidi kuwa, nimesoma na kuyaelewa masharti yote ya kukaa hosteli na kwamba nitafuata na kuyazingatia yote. Ikiwa nitakiuka mojawapo ya haya masharti niondolewe hosteli mara moja.

_____ _____

Sahihi ya Mwanafunzi Sahihi ya Mzazi

_____

Mhuri wa Mkuu wa Shule.